OFISI YA RAIS TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA NAMTUMBO

Anwani ya simu……
Simu Na. **0621057336 /0673158778/0752 648868**
Unapojibu tafadhali taja

Shule ya Sekondari ya Nanungu
S.L.P 701
Songea
Tarehe: 26.05.2021

Kumb. Na. NNSS/US/FV.03/2021
Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……
S.L.P ……

YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NANUNGU KWA MASOMO YA KIDATO CHA TANO MWAKA 2021 – 2022</u>

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Nanungu ipo umbali wa kilometa moja na nusu kutoka Barabara ya Songea Njombe, kwa anayetoka Njombe, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya na Mikoa mingine ya ukanda huo. Shule ipo katika Kijiji cha Mlilayoyo umbali wa kilometa 25 kutoka mji Mkuu wa Halmashauri / Mkoa Ruvuma. Usafiri wa basi kutoka Songea mjini kuja Shule unapatikana katika kituo cha daladala **Songea mjini** au Stendi kuu ya mabasi SHULE YA TANGA nauli shilingi 1000/=.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 04.07.2021, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shule kati ya tarehe 04.07.2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 30.07.2021.NB: ZINGATIA TANGAZO LA SERIKALI LA KURIPOTI SHULENI.

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-**
   - **a) Sare za Shule**
     - i. Masharti mawili (2) rangi nyeupe tetroni mikono mirefu.
     - ii. Fulana nyeupe ya kuvalia kwa ndani
     - iii. Sketi mbili (2) rangi nyekundu damu ya mzee aina ya mshono wa rinda box isiyo na V pembeni malinda madogomadogo iwe ndefu kufikia enka ya miguu (Kifundo cha mguu).
     - iv. Jozi mbili (2) za viatu vya ngozi vyeusi visivyo na visigino virefu na vya kufunga kamba.
     - v. Jozi mbili za soksi nyeupe ndefu (stocking)
     - vi. Sweta mbili nyekundu damu ya mzee zinapatikana madukani.
     - vii. Nguo za kazi ni gauni la heshima lisilobana na livuke magoti rangi ya kijani kibichi (shamba dress).
     - viii. Kwa wasichana wa kiislamu vazi la Msikitini ni hijabu nyeupe nusu kanzu tetroni isiyo angaza suruali pana rangi ya blue bahari.
     - ix. T-shirt zenye nembo ya Shule zinapatikana hapa Shuleni kwa ghalama ya Tshs. 12,000/= (Pesa hii utalipa pale unapokabidhiwa T – Shirt)
     - x. Nguo za michezo raba, bukuta, sketi na jezi rangi nyekundu au bluu(Isiwe na maandishi).
     - xi. Tracksuit rangi ya kijani ufito mweupe ni lazima iwe pana tafadhali.
     - xii. Begi la kubebea daftari “School bag” rangi nyeusi
     - xiii. Tai Rangi ya damu ya mzee kama rangi ya sketi.
     - xiv. Sketi ya rangi ya khaki (amerika) mshono kama ule wa sketi ya damu ya mzee huvaliwa baada ya vipindi vya darasani.

NB: Mwanafunzi atakaguliwa vifaa vyote afikapo shuleni.

<u>HAIRUHUSIWI</u>

i. Vazi lingine lolote nje ya sare za shule likivaliwa Shuleni hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.
ii. Herein, mikufu, pete, shanga, bangili n.k. haviruhusiwi kuvaliwa Shuleni.
iii. Hairuhusiwi kupaka rangi kucha, wanja machoni au kujichubua kwa mkorogo
iv. Kusuka nywele mtindo wowote

NB: Haturuhusu vazi lingine Shuleni zaidi ya uniform.

b) ADA NA MICHANGO YA SHULE

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **20,000/=** kwa mwanafunzi wa kutwa na shilingi **70,000/=** kwa mwanafunzi wa bweni. Unatakiwa kulipa kiasi cha shilingi **10,000/=** kwa mwanafunzi wa kutwa kwa muhula na shilingi **35,000/=** kwa mwanafunzi wa bweni kwa muhula. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **Na. 62401100029** katika Benki **ya NMB JINA LA AKAUNTI NI NANUNGU SEKONDARY SCHOOL.** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay slip).

b) Michango inayotakiwa kulipwana kila mzazi ni:-
i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa thamani.
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho.
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 30,000/= kwaajili ya kulipia wapishi walinzi na vibarua wengine.
v. Shilingi 2000/= nembo ya Shule.
vi. Shilingi 25,000/= kwaajili ya huduma ya kwanza ya afya.
vii. Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima (Mock)
viii. Shilingi 5,000/= fedha ya tahadhali (haitarejeshwa)
ix. Shilingi 50,000/= MChango wa dawati na kiti .

MPANGILIO WA ULIPAJI WA MICHANGO HII YA HAPO JUU UFUATE JEDWALI HILI HAPO CHINI

MUHULA I		**MUHULA WA II**	
Ada	Tshs. 35,000/=	Ada	Tshs. 35,000/=
Dawati na kiti	Tshs. 50,000/=	Taaluma	Tshs. 10,000/=
Taaluma	Tshs. 10,000/=	Wapishi	Tshs. 15,000/=
Ukarabati	Tshs. 15,000/=	Huduma ya kwanza	Tshs. 10,000/=
Wapishi	Tshs. 15,000/=	Mahafali FVI	Tshs. 5,000/=
Kitambulisho	Tshs. 6,000/=		
Nembo	Tshs. 2,000/=		
Huduma ya kwanza	Tshs. 15,000/=		
Tahadhari	Tshs. 5,000/=		
Mahafali F IV	Tshs. 5,000/=		
Jumla	**Tshs. 158,000/=**	**Jumla**	**Tshs. 75,000/=**

2. Jumla ya michango yote kwa bweni ni <u>Tshs. 233,000/=</u> kwa mwaka.

3. MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI:-
i. Ream ya karatasi moja kwa kila muhula.
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
iv. Scientific calculator (FUNCTION Fx 991 ms2, 401) Pia zinapatikana ktk dukala shule kwa shs 40,000/ tu.
v. Godoro (ukubwa 2 ½ kwa 6)
vi. Shuka 2 blue bahari, blanketi 1, chandarua 1, foronya 1, mto 1.
vii. Vyombo vya chakula sahani, bakuli, kijiko na kikombe.
viii. Ndoo kubwa 1 na ndogo 1 zenye mifuniko.
ix. Mopa , jembe (lenye mpini), reki 1, fagio la ndani (laini) 1 na la nje 1 (chelewa).
x. Taulo, mswaki, sabuni, mafuta, kitenge doti 1.
xi. Tranka (sanduku la chuma/bati) la kuwekea vifaa vyake.
xii. Madaftari Counter books 10 na mathematical set.

xiii. Fedha zake kwa matumizi binafsi (zitahifadhiwa na walezi).
xiv. Vitabu vinavyomfaa kununua inapobidi rejea ukurasa wa mwisho
xv. Faili mojo kwa ajili ya kutunzia kumbu kumbu zake

4. MAKOSA YATAKAYO MSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:-

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha migomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu, au mtu yoyote Yule.
vi. Ulevi na unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
vii. Uvutaji sigara.
viii. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
ix. Kupata au kutoa mimba.
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xi. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xii. Kumiliki au kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya Shule.
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv. Kudharau bendera ya Taifa.
xv. Uharibifu wa mali ya uma kwa makusudi.

5. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examinational fomu) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayo tolewa na Shule.
d) Picha passport 4 za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanao weza kumtembelea mwanafunzi Shuleni pamoja na namba zao za simu na passport size 4 za mwanafunzi .
e) Aje na **Result slip original** na copy yake pamoja na cheti cha kuzaliwa (Photocopy) vitakaguliwa ofisi ya taaluma.

6. Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo na kutekeleza kikamilifu.

MENGINEYO

i. Ikipita tarehe 30/07/2021 kama haujaripoti shuleni utakuwa umepoteza nafasi yako.
ii. Mzazi wa mwanfunzi anayohaki ya kufuatilia mahudhurio, maendeleo,tabia na mwenendo wa mwanafunzi shuleni kwa kuwasiliana na Ofisi ya Mkuu wa shule.
iii. Wageni wa wanafunzi wakati wapo shuleni lazima waonane kwanza na mwalimu wa zamu / wa Darasa/ Bweni au Matroni ambaye amepewa uwezo wa kukubali au kutokubali kuonana na mwanafunzi.
iv. Siku za kuwaona wanafunzi ni wikiendi za mwisho wa mwetu tu.

v. Huruhusiwi kuja na vitu vifuatavyo shuleni:
(a) **Simu ya mkononi** (mawasiliano yote yatafanyika kwa utaratibu uliowekwa na shule).
(b) Pasi ya umeme.
(c) Masanduku makubwa nje ya tranka hakuna nafasi bwenini.
(d) Nguo zisizo za shule.
(e) **Ukija navyo utarudisha nyumbani kwa gharama zako mwenyewe au vitachukuliwa**.

MATUMIZI NA UTUNZAJI WA MALI ZA SHULE NA MAZINGIRA

a) Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia na kutunza mali ya shule kama vile majengo, viti meza, madawati majembe, ndoo vitabu, vifaa vya maabara n.k.
b) Hakikisha kwamba taa za umeme zimezimwa wakati wote mchana.
c) Kisima cha maji kifunikwe baada ya matumizi.
d) Weka mazingira ya shule kuwa safi na ya kuvutia, okota karatasi na uchafu wote. Pita kwenye njia za miguu, na usikatishe kitishe ovyo na kukanyaga maua au majani yaliyooteshwa.

UTORO

Mwanafunzi ambaye hatahudhuria shuleni bila taarifa atahesabiwa kuwa ni mtoro kuhusu mwanafunzi asiyehudhuria shuleni kutokana na matatizo yoyote lazima taarifa ziwasilishwe shuleni siku hiyo ya matatizo kwa mwalimu wa zamu au walimu wa malezi na Mzazi/ Mlezi anayetambuliwa na shule kulingana na fomu za usajili.

MASHARTI YA KUJIUNGA NA BWENI

Pamoja na sheria na kanuni muhimu za shule unapaswa

i. Kukubaliana na sheria na kanuni zote za shule
ii. Kufuata ratiba ya siku kwa mwanafunzi wa bweni
iii. Kuhudhuria “Roll – calls” zote kama inavyopangwa na walezi.
iv. Kuhudhuria “Prepo” na vipindi vyote vya darasani
v. Kuishi kwa amani upendo na ushirikiano wa kidugu na wanajumuiya wote
vi. Kula “Menu” moja iliyoandaliwa na Shule bila kuleta usumbufu wa kujichagulia chakula CHAKULA KIKUU HAPA NI UGALI NA MAHARAGWE.
vii. Kuchangia gharama za matengenezo ya uharibifu wowote inapolazimu
viii. Kutomleta au kumwingiza mgeni yeyote ndani ya bweni (wanafunzi wa kutwa ni miongoni mwao).
ix. Kutoleta au kukaa ndani ya bweni bila ruhusa ya walezi wakati wa masomo
x. Hauruhusiwi kupika chochote
xi. Ni marufuku kwa wanafunzi wavulana kuingia bweni la wasichana.
xii. Kutolala nje ya shule bila kibali maalumu cha utawala
xiii. Kuvaa sare ya shule wakati wote wa vipindi na awapo nje ya mipaka ya shule (kwa shughuli binafsi, shule au kidini”).
xiv. Kuvaa sare baada ya saa za masomo ndani ya mipaka ya shule shati na t-shirti ya shule na sketi ya khaki America.
xv. Zingatia UHURU WA KUABUDU “Kumcha MUNGU ni chanzo cha maarifa, hekima, busara, utu wema, uadilifu, upendo, amani na uaminifu”. Unaruhusiwa kuabudu kwa kadili ya dini yako ila usivunje sheria na taratibu zilizowekwa hapa shuleni.

Ninakutakia maandalizi mema na kuwakaribisha wote mzazi na mwanafunzi katika jumuiya ya shule.

……..
HEADMASTER
NANUNGU SECONDARY SCHOOL

WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA

SHULE YA SEKONDARI NANAUNGU

FOMU YA KUKUBALI (FOMU HII IRUDISHWE SHULENI)

1. Mimi …….. kidato cha ……..mimekubali kujiunga na shule ya Sekondari Nanungu nikiwa mwanafunzi wa bweni.
2. Ninakubali masharti yote, na ninaahidi kufuata sheria zote za shule.
3. Niko tayari uongozi wa shule kuchukua hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunirudisha kwa mzazi/mlezi endapo nitakiuka masharti yaliyomo au kubainika kuwa na afya isiyoridhisha ambayo itahitaji ukaribu na matunzo ya mzazi au mlezi mwenyewe.
4. Sahihi ya mwanafunzi ……. Tarehe…….

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

1. Mimi ……ninakubali mtoto wangu …….. wa kidato cha ……... mwaka ……kujiunga na sekondari ya Nanungu kuanzia tarehe…….. akiwa mwanafunzi wa bweni.
2. Ninakubali masharti yaliyomo katika kujiunga na bweni ikiwa ni pamoja na kulipa karo yote ya shule na kumtimizia mahitaji mengine ya shule.
3. Nitakuwa tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka masharti yaliyomo au kubainika kuwa na afya isiyoridhisha ambayo itahitaji ukaribu wa matunzo ya mzazi/ mlezi mwenyewe.
4. a) Anuani ya kudumu ni
   ……
   ……
   ……
   b) Jina na anuani ya mlezi wa karibu mjini ambaye shule inaweza kuwasiliana naye katika matatizo mbalimbali ya mtoto ni
   ……
   ……
   ……..
   ……..
5. sahihi ya mzazi/mlezi ……..tarehe……..

SHULE YA SEKONDARI NANUNGU

FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI

1. Jina kamili ……..
2. Mahali ulipozaliwa …….
3. Tarehe ya kuzaliwa ……
4. Uraia ……
5. Anuani ya nyumbani …….
6. Jina la mzazi/mlezi ……..
7. Anunani ya mzazi/mlezi (kama tofauti na hiyo hapo juu) ……
8. Ndugu wa karibu. Anuani yake, kitongoji /mtaa ……

	Jina	Uhusiano	Anuani yake	simu
1.	……..	……..	……..	……
2.	……..	……..	……..	……
3.	……..	……..	……..	……
4.	……..	……..	……..	……

9. Dini ……
10. Kidato alichopokelewa ……
11. Shule uliyotoka ……..
12. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, kuimba n.k …….
13. Wilaya unakotoka ……mtaa ……..kata……..
14. Sahihi ya mwanafunzi ……tarehe……
15. Sahihi ya mzazi/mlezi……tarehe……

Matumizi ya ofisi

Namba ya shule …….

Namba ya mtihani ……..

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

NANUNGU SECONDARY SCHOOL

P.O. BOX 701

SONGEA

To be completed by medical officer
Full name ……
Age …….. Years …….. Sex……
Blood count (Red and White) …….
Stool examination …….
Urine analysis ……..
Syphilis test ……
T.B test …….
Ears ……..
Chest ……..
Spleen ……
Abdomen …….

Additional information eg. Physical or chronically family
Disease, etc ……
……
……..
I certify that the above-named student is fit to persue studies
Signature ……
Designation ……
Section ……
Date ……..
NOTE; Medical officer at the time of examination the individual any aliments you note PUPILS.
You must bring complete form when you come to school, no pupils may enroll without certificate of physical fitness.

……..
HEADMASTER
NANUNGU SECONDARY SCHOOL

ORODHA YA VITABU AMBAVYO MZAZI ANAWEZA KUVINUNUA KWA AJILI YA MWANAE ILI AJISOMEE YEYE BINAFSI

a. Chemistry

(i) Advance level organic by APE network 2012"
(ii) A' level secondary Education chemistry practical
(iii) Advance inorganic chemistry volume I and II by S. CHAND
(iv) Environmental chemistry and pollution control by S. CHAND
(v) Essential physical chemistry by S. CHAND
(vi) Selected topic in inorganic chemistry by Wahid .U. Malik et at
(vii) Organic Chemistry by S. CHAND.

b. Biology

i) CJ CLEGG with DG MACKEAN (2000) Advanced Biology principle and Application 2nd ED, Hodder Murray London.
ii) Syvia S Mader (1996), Biology (5th ED) Wm C, Brown Publisher London
iii) DJ Taylor et al (1997), BIOLOGICAL SCIENCE, Cambridge University press – New York.
iv) MBV Roberts (1986), Biology A functional Approach (4th ED)
v) Ann Fullick et al (2011), A level Biology, students Books, Longman

c. General studies

i) General studies for Level Certificate form V BY. RICHARD MBALASE
ii) General studies for A'level certificate from vi. BY RICHARD R. MBALASE.

d. Geography

i) Practical geography Alive By Zisti
   - Map Reading, photography interpretation, Field Research, Statistics, and survey by Ellis Anthony Mkoko.
   - Affordable Edition for Secondary and High School learners kot publisher

ii) A comprehensive approach to physical and high school learners kot publisher.
iii) Human and economical geography by GILLAN.C. MARGAN
iv) Soil and climatology by zisti.
v) Principle of Physical Geography by F.J Monk House
vi) Geography integrated approach by: D. Wough
vii) General geography in diagrams by R.B Burnet
viii) Statistical methods and the Geographers by S. Gregory
ix) Geography 1 & 2 questions with answers (Review) by Msabila / Nyambari.

ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO

1. HISTORY

i. Modern World History by Ben Walsh
ii. African in the World History by Nyirenda
iii. The Russian Revolution and the Bolshevik Victory by D.C Heath and company
iv. Major events in the African History y Fr. Kamara.

2. ENGLISH

i. English for Advanced Level Dr. Kadeghe
ii. Advanced English Dictionary – Oxford University
iii. Selected poems from East Africa by TIE and other poems text books.
iv. The beautiful ones are not yet born our Ayi Kwai
v. A man of the people by Achebe
vi. Death of sales man – Henry Ibsen
vii. Rwanda Magere – Okoit Omtata
viii. The bride price by Austine Bukenya

3. KISWAHILI

i. Nadharia ya Lugha – Masebo
ii. Nadhari ya fasihi – Masebo
iii. Nadharia ya Lugha – Saluhuya, C.
iv. Fasihi maswali namajibu kidato cha tano na sita – Masebo.
v. Kamusi ya Kiswahili sanifu.